


Mifumo ya kidijitali yaimarisha huduma za afya barani

Barani Afrika, watu wengi hasa sehemu za mashambani, wanalazimika kusafiri mbali kufikia vituo vya matibabu na hivyo huduma za za kidijitali zitawafaidi pakubwa

NA PAULINE ONGAJI
pongaji@ke.nationmedia.com

AKIWA nyumbani kwake katika kijiji cha Nangina Kaunti ya Busia, Bi Isabella Wangila (sio jina lake kamili) anapokea maagizo kuhusu jinsi ya kufuatilia ratiba yake ya matumizi ya dawa, kutoka kwa daktari, kupitia arafa za rununu.

Tangu agundulike kwamba anaugua maradhi ya shinikizo la damu, Bi Nangina amekuwa akipokea huduma hii kutoka kwa daktari jijini Nairobi.

Matumizi ya teknolojia hii kufikia huduma ya afya imemrahisishia mambo, vile vile kumuokelea muda na mapeni.

"Ilikuwa changamoto kwangu kupokea huduma kwani siishi karibu na hospitali, na pia hata wakati ambapo nilikuwa nikipata fursa ya kufika hospitalini, ilikuwa shida kutibiwa kutokana na uhaba wa madaktari na wahudumu wa afya,"aeleza.

> **Matumizi ya huduma za afya kupitia majukwaa ya kidijitali yataimarisha huduma za afya na kuwawezesha Wakenya kutoka maeneo yote kufikia huduma bora za afya.**
> **-Dkt Radha Karnad (HealthX Africa)**

Masaibu yaliyokuwa yakimkumba Nangina, ni taswira inayowakabili wagonjwa wengi sio tu hapa Kenya, bali Afrika nzima.

Utafiti unaonyesha kwamba barani Afrika, idadi kubwa ya watu hawafikii huduma za afya wanazohitaji. Udadisi uliokusanywa kati ya Novemba 2020 na Machi 2021, kuhusu hali ya huduma nafuu ya afya kwa wote barani ulionyesha kwamba ni asilimia 48 pekee ya idadi ya watu katika mataifa yaliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanapokea huduma za afya wanazohitaji, huku hali ikiwa mbaya hata zaidi kwa wale wanaoishi katika sehemu za mbali za mashinani.

Humu nchini, takwimu zinaonyesha kwamba kuna takriban vituo 13,517 vya umma na kibinafsi vya afya, idadi ambayo ni ndogo sana kwa idadi ya watu ambayo ni milioni 50 na inaendelea kukua.

Isitoshe, sekta ya afya aidha inakumbwa na tatizo la uhaba wa madaktari na wahudumu wengine wa afya. Kufikia mwaka wa 2019, idadi ya madaktari waliosajiliwa nchini ilikuwa 12,090, ambayo ni sawa na madaktari 25 kwa kila watu 100,000, kiwango ambacho ni cha chini sana kikilinganishwa na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani WHO ya daktari mmoja kwa watu 1,000.


Kulingana na wataalam wa afya, mojawapo wa suluhu za kukabiliana na changamoto hizi, ni matumizi ya mbinu za kidijitali katika huduma za afya, hasa kwa raia wanaoishi mashambani.

Nchini Kenya baadhi ya mifumo hii ya kidijitali inahusisha usafirishaji wa dawa na bidhaa za afya, apu za simu za rununu, uhifadhi wa rekodi na stakabadhi za wagonjwa kwa njia ya kieletroniki, na ushauri kutoka kwa

TAKWIMU

1,000

Shirika la Afya Duniani WHO linapendekeza daktari mmoja kwa watu 1,000.





wahudumu wa afya kupitia mifumo ya kidijitali.

Teknolojia hizi zinatumika kwa mfano kuwezesha wataalam wa afya na wagonjwa kuwasiliana pasipo kukutana ana kwa ana, kufuatilia afya ya mgonjwa, kuunda mpangilio maalum wa mgonjwa na kuhifadhi data za wagonjwa kupitia mfumo wa kidijitali.

Matumizi ya mifumo wa kidijitali kutoa na kufikia huduma za afya humu nchini, yalishika kasi hasa baada ya mchipuko wa gonjwa la COVID 19 mwaka wa 2020, ambapo kutokana na marufuku ya kututoka nje, madaktari na wahudumu wa afya walianza kutoa huduma kupitia majukwaa haya.

Hii ilichochea baraza la madaktari na wahudumu wa afya, vilevile baraza la madaktari wa meno nchini, kuchukua hatua na kuanza kuidhinisha taasisi mbali mbali za kimatibabu kutoa huduma za afya kupitia majukwaa ya kidijitali.


"Matumizi ya huduma za afya kupitia majukwaa ya kidijitali yataimarisha huduma za afya na kuwawezesha Wakenya kutoka maeneo yote kufikia huduma bora za afya,"asema Dkt Radha Karnad, kutoka HealthX Africa, jukwaa linalotoa huduma za kiafya kupitia mifumo ya kidijitali nchini.

KWA UFUPI

Matumizi ya mifumo dijitali

Matumizi ya mifumo wa kidijitali kutoa na kufikia huduma za afya humu nchini, yalishika kasi hasa baada ya mchipuko wa gonjwa la COVID 19 mwaka wa 2020, ambapo kutokana na marufuku ya kututoka nje, madaktari na wahudumu wa afya walianza kutoa huduma kupitia majukwaa haya.

Hii ilichochea Baraza la madaktari na wahudumu wa afya, vilevile baraza la madaktari wa meno nchini, kuchukua hatua na kuanza kuidhinisha taasisi mbali mbali za kimatibabu kutoa huduma za afya kupitia majukwaa ya kidijitali.



Tayari mbinu hizi zinatumika pakubwa katika mataifa mengine barani. Nchini Malawi, Villagereach, shirika linalofanikisha matumizi ya teknolojia kutoa huduma za afya limeshirikiana na serikali ya nchi hiyo kuzindua nambari maalum ya simu, inayowawezesha watu kupiga simu bila malipo, na kupata taarifa za kweli za afya kutoka kwa wahudumu wa afya waliofuzu.

Kupitia jukwaa hili, simu za rununu zinatumika kuwasilisha taarifa za kiafya, vile vile kuunganisha wahudumu wa afya na wagonjwa, na hivyo kuhakikisha kwamba wagonjwa hata katika sehemu za mashinani wanafikiwa.

Katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo DRC, kupitia VillageReach, hospitali za maeneo ya mbali zimekuwa zikiletewa bidhaa muhimu za kimatibabu kama vile chanjo, damu na dawa za wanawake wajawazito na watoto, kwa kutumia mitambo ya droni.

"Tunafurahia kwani kabla ya mpango huu tulikuwa tunachukua muda mrefu kusafirisha chanjo ya maradhi ya kupooza (polio), suala lililokuwa likiathiri ubora wake,"aeleza kiongozi wa jamii katika kituo cha afya cha Maanga, eneo la Bikoro nchini DRC.

Hapa Kenya, shirika la Villagereach limeshirikiana na Wizara ya Afya katika masuala ya upanuzi na ufikiaji huduma za dharura za simu. Ushirikiano huu unahusisha jinsi ya kukabiliana na mkurupuko wa maradhi ya kupooza (polio).

"Hasa tumekuwa tukihusika na shughuli za kuimarisha shughuli za usafirishaji wa sampuli za wagonjwa wa polio, na hivyo kuhakikisha kwamba zinawasilishwa kwa ubora wa hali ya juu, kutoka vituo vya afya vya kijamii, hadi katika maabara ya kitaifa na kimataifa," aeleza Bw Edwin Mulwa, mkuu wa masuala ya kidijitali katika shirika la Villagereach.

Kulingana na Dkt Karnad, mifumo hii inawezesha wagonjwa kufikia huduma za afya bora haraka na bei nafuu. "Aidha, inawapa wagonjwa uwezo wa kufuatilia rekodi zao za afya, na pia kuwawezesha kufikia huduma za afya mapema."

Lakini haimaanishi kwamba mifumo hii ndio suluhu kamili ya tatizo la huduma za afya barani, hasa ikizingatiwa kwamba pia inakumbwa na udhaifu.

"Sekta hii inakumbwa na changamoto kama vile kutokuwepo kwa udhibiti hasa ikizingatiwa kwamba kuna baadhi ya vituo ambavyo havijaidhinishwa kutoa huduma hii, ilhali vinaendelea na shughuli,"aeleza.

Pia, kulingana na mtaalam huyu, majukwaa ya kutoa huduma za afya kupitia mifumo hii, hayana mpangilio, na hivyo kufanya wagonjwa wakose imani na huduma hizi.

"Teknolojia aidha inaimarika kwa kasi ikilinganishwa na udhibiti, kumaanisha kwamba kuna haja ya serikali na mashirika kama vile Digital Health Agency, kuhakikisha kwamba sera za udhibiti zipo."

Na ndiposa wataalam wa afya wanaendelea kusisitiza kwamba sekta ya huduma ya afya bado inahitaji wagonjwa kuhudumiwa hospitalini na wahudumu wa afya.

"Katika hali nyingi wagonjwa watahitaji kuonekana na daktari ana kwa ana, na kufanyiwa uchunguzi. Aidha, kuna baadhi ya huduma maalum za upasuaji zinazohitaji daktari kumuona mgonjwa ana kwa ana."

Hata hivyo, kulingana na wataalam, mtazamo wa siku zijazo wa huduma za afya hasa barani utategemea na mifumo ya kidijitali ya kutoa huduma za afya.

"Nchi zinazostawi kama Kenya hazitatimiza ndoto ya afya kwa wote kufikia mwaka wa 2030, ikiwa mifumo ya kidijitali haitachukuliwa kwa umakini. Hii ni hasa ikizingatiwa kwamba hatuna rasilimali za kujenga hospitali na vituo vya afya vya kutosha ili kukabiliana na idadi kubwa ya watu inayozidi kuongezeka. Aidha, tunakumbwa na uhaba wa wahudumu wa afya,"aeleza.